MDUARA NA MSTARI

MWONGOZO KUFIKIA UHURU KWA NJIA YA MSALABA.

Na CHARLES R. SOLOMON , E d. D.

Unaposoma hii , waweza kuwa katikati ya msukosuko . Mtu pengine alikosa kufanya alivyokuahidi na Mungu akaonekana mbali sana asiweze kukusaidia . Labda umepevuka ukijiona hupendwi kwa kiwango cha kutimiza mahitaji yako . Yawezakana hujawai kujikubali na kujipenda mwenyewe .

Hali ya upungufu mtu anaweza kujiona anayo katika kukabiliana na maisha yaweza kuanzia huzuni wa kiasi wa ndani na hatimaye mawazo yakujinyonga . Kwa ajili hii , uhusiano wako na wale uwapendao waweza umefika hatua ya kuvunjika au tayari umevunjika usiweze kurudishwa . Kama upo katika hali ndogo yakukata tamaa au kabisa umekufa moyo , ujumbe huu ni kwa ajili ya hali yako .

Mungu alikupenda kiasi cha kutuma Mtu - Mwanawe , Bwana Yesu Kristo &endash; kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako , kumfufua tena , na kutoa kupitia yeye yote ambayo ni muhimu kwa ushindi ,na maisha tele . Leo waweza kuamini kuwa kifo chake kilitimiza sharti la Mungu wa msamaha bure wa dhambi zako au huamini . Kama huamini , ujumbe huu rahisi , na michoro ya kueleza , unaweza kubadilisha maisha yako unapopokea Maisha Yake &endash; Uzima wa Bwana Yesu Kristo .

Inawezekana umemwamini Kristo kwa wokovu wako lakini sasa wewe ni mwamini anayekakamka , na aliyeshindwa na bado hujapata njia ya ushindi katika maisha ya Kikristo.

Iwapo mojapo ya hali hizi zinaeleza hali yako , tafadhali soma kwa makini mawazo yafuatayo na Bibilia wazi pamoja na maombi ili Mungu akuangazie kweli hii .

Umbo Lako

Mchoro wa Mduara waonyesha mtu akiwa wa sehemu tatu ambazo ni , roho , nafsi , na mwili (1 Wathesalonike 5: 23) . Kwa mwili

kupitia hisia , tunahusiana na mazingira yetu. Nafsi , yajumuisha utendaji kazi wa nia , uchaguo na maono . Nafsi hutuwezesha kuhusiana mmoja kwa mwingine . Roho hutuwezesha kuinuka juu ya uweza wetu , vizuizi na hali zote tunapozaliwa mara ya pili na Roho Mtakatifu kukaa ndani yetu.

Roho yaweza kuwa na uhusiano na Adamu &endash; familia ya Shetani (tazama mchoro wa mstari) - au na Kristo , familia ya Mungu . Tunazaliwa duniani kama wazao wa Adamu na washiriki wa asili yake. Yamaanisha roho zetu zimekufa kwa Mungu na hai kwa Shetani. Tumo katika familia isiyofaa ! Kwa vile maisha yetu yalitoka kwa baba yetu wa kwanza , Adamu , na kurudi nyuma katika mnyororo usiokatika kwake , tulikuwa hakika ndani yake tulipotenda dhambi . Hivyo, tulifanyika wenye dhambi kabla kuzaliwa katika mwili huu. Kwa hivyo, tunafanya tu yale ya asili tunapotenda dhambi (Warumi 3: 23) . Kila maisha yanayobakia katika Adamu mwishowe yataishia Kuzimu , kama inavyoonyeshwa katika mchoro (Warumi 6 : 23) . Ingawa tunaweza ishi maisha mazuri sana , kusema kibinadamu , tumetengwa kwa Mungu ijapokuwa na hadi tutakapozaliwa katika familia yake kwa kuzaliwa kiroho.



Mchoro wa Gurudumu

FAHAMU: Sura ya kwanza katika kitabu &endash; Handbook to Happiness and You - a Spiritual Clinic (Akijatafsiriwa katika kiswahili) , yakuruhusu kutumia mafundisho haya unapomhoji mtaka ushauri , ukitumia kitabu hicho wewe kama Mshauri .

Mahitaji Yako

Neno " wokovu" (1) katika mchoro wa mduara yamaanisha lazima tuzaliwe kiroho . Ni kwa njia hii pekee tunaweza kutoka katika maisha ya Adamu na kuzaliwa katika maisha ya Kristo , ambayo ni uzima wa milele , ilivyoonyeshwa katika Mchoro wa Mstari (Yohana 3 :3) . Kuzaliwa kiroho, ni lazima tutambue au kukiri kwamba tumo katika maisha maovu na kwa hivyo tumezaliwa wenye dhambi , na matokeo yasioepukika yakuwa tumetenda dhambi . Kwa hivyo lazima tumkubali Kristo katika maisha yetu , kwa sababu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu .

Kwa kuzaliwa kiroho , wanaompokea Roho wa uzima wa Kristo

katika roho zao kwa imani wanaungwa roho moja naye (1Wakorintho 6: 17) . Ikiwa watapata ushindi juu ya majaribu na kufurahia amani ya Mungu maishani , hata hivyo , ni lazima wawe na uhakika wa wokovu wao .

Uhakika (2) lazima msingi wake uwe katika ukamilifu wa neno la Mungu lisilokuwa na makosa , au utatoweka kwa vyo vyote .

Wengi wanaofahamu (na nia zao) kwamba wenyewe wamemuamini Bwana Yesu Kristo bado wanakosa ukweli wa uhakika kwa sababu hawajawi kusikia wameokoka . Kutokana na migongano ya maono , baadhi inayotokana na kukataliwa tangu utoto , hisia za mtu (au maono) mara chache hukubaliana na kweli , jinsi kweli ile imeelezwa katika Bibilia au ilivyo duniani . Jinsi tunavyo hisi mambo inaweza kutofautiana na hali ya kweli ya mambo hadi Kristo awe mtu wa katikati ya maisha yetu na kuponya maono yaliyoharibiwa .

Mwamini , awe wazamani au mpya , lazima afahamu huingia katika uhusiano salama , wa kiroho na wamilele pamoja na Mungu kupitia Bwana Yesu Kristo (Yohana 5:24) na kwamba anaweza kutegemea na kufurahia huo usalama (3) . Ijapokuwa wamini wengi wanafahamu wamemkubali Kristo , wachache wanaelewa na kufurahia ukweli kwamba wamekubalika ndani yake . Wengi wamelazimika kupata ukubali kwa misingi ya binadamu na kuhisi kwamba lazima pia kwa juhudi yao washiriki ukubali (4) wa Mungu , ingawa tayari wamekubaliwa kabisa kupitia maisha ya Kristo yaliyo yao . (Waefeso 1:6) . Kila mwamini amekubalika , lakini wengi hawakubali ukubali wao , au haki . (2 Wakorintho 5:21) , kwa imani .

Wachache , pia , ni wale ambao hujitoa kamilifu (5) au kujisalimisha maisha yao yote kwa Bwana Yesu Kristo . Huu ni uamuzi usiobadilika ambapo tunaruhusu Mungu kutenda lolote atakalo ndani yetu , nasi , kwetu au kupitia kwetu . Tunatoa haki zetu zote .

Mara kwa mara , hali hugeuka na kukaribia mchafuko baada kufanya uamuzi kama huo , kwa sababu Mungu huheshimu ombi letu kwake kuchukua uongozi kamili wa maisha yetu . Ikiwa atachukua uongozi ni lazima sisi tupoteze uongozi , ni hii ndiyo hatua mara chache hutupa furaha ! Hali au watu Mungu hutumia kutuelekeza mwisho wa uongozi wa maisha yetu mara nyingi sio ya kiroho . Wakati mwigine huja na mateso yasiyostahili , lakini ni mateso aina hii yanayokamilisha kusudi la Mungu maishani mwetu (1Petro 2:20-21; Wafilipi 1:29,30) . Wakati wa mateso au

kuadhibiwa (Wafilipi 3:10; Waebrania 12:11) , ni mara chache kuona sababu ya furaha , lakini ndiyo yanayozaa utakatifu tunaotamani . Makusudi ya Mungu kwa mwamini ni kumfananisha na mfano wa Kristo (Warumi 8:29) . Kufananishwa huku hujumuisha mateso . Neno " mambo yote "ya Warumi 8:28 hufanya kazi pamoja kwa uzuri ni shida kuonekana ina uzuri ila kukumbuka yaliyopita .

Mgongano wa Kindani

Herufi " U" katikati ya mduara yawakilisha maisha ya kujiongoza au "mwili ". Mwili umetawala maisha ya wamini wengi katika ukristo wao wote . Hutafuta maumbile tofauti , ikitegemea mtu mwenyewe , kufikia timizo la mahitaji yake kwa kitu fulani au mtu kwa njia isiyokubalika ama inayokubalika . Fedha , vitu vya mwili , mafanikio , sifa , ngono , mamlaka au baadhi ya vitu vingine visivyohesabika vinaweza kuendesha ama kuvutia mtu na kufanyika kitu cha muhimu sana anapotawaliwa na maisha ya ubinafsi au mwili . Hivyo " mwili " ni kujaribu kwa mwamini kuishi maisha ya kikristo kwa nguvu zake . " Mwili " kwa hivyo ni tatizo zito sana kwa mkristo - sawa na ibada ya sanamu . Kwa sababu tunapobadilisha umuhimu wa Kristo na kitu chochote - hata sisi wenyewe - chochote tunachoweka katika kiti cha enzi ya maisha yetu hufanyika sanamu . Mungu lazima ashugulike kwa nguvu na mwili wetu . Ndivyo afanyavyo , kawaida kwa kufichua kutokuweza kwa maisha ya ubinafsi kufaulu hadi mwamini akishapata hali haivumiliki ujisalimisha na kutaka kubadilisha maisha ya ubinafsi kwa maisha ya Kristo .

Kadiri ubinafsi au (mwili) unapoendelea kuongoza , migongano inayoonyeshwa katika " nafsi " (utu) wa mchoro wa mduara itaendelea . Inaweza kuwa mbaya zaidi kufuatana na umri na kuongezeka kwa majukumu .Wakati mwingine , maisha ya ubinafsi yaliyorekebishwa vizuri kisaikolojia yanaweza kuhimili na hali kwa muda mwingi wa maisha , bali matokeo hayawezi kutosheleza .

Upungufu wa kisaikolojia , pamoja na hatia (halisi na yakuwaza) , huungana na kuleta viwango mbali mbali vya pingamizi katika maisha ya kujiongoza . Pingamizi hii lazima ishugulikiwe . Wengine huchagua kuwalaumu wengine kwa kutumia mapigano - ya mwili au kwa maneno - ambapo wengine ni waoga zaidi kwa kulipizwa kisasi na unyamazisha uadui wao vema wawezavyo . Wengine hunyamazisha hasira na pingamizi kwa sababu wanajilaumu kwa kila tatizo na udhia wanayokutana nayo . Wakati uadui na pingamizi unanyamazishwa , kwa sababu yeyote ile ,

italeta madhara katika nia au maono au yote mbili. Uadui au hasira wa kindani kawaida matokeo yake ni huzuni na / wasiwasi katika maono . Watu wengine wanaweza kutumia nia zao kufanya uharibifu wa aina mbali mbali au kukana ukweli . Hii inawawezesha kukwepa sharti la kushugulikia tatizo la kweli , maisha ya ubinafsi .

Wakati mgongano wa kisaikolojia unapokokota bila ponya , walakini , kawaida matokeo yake ni magonjwa mwilini , vile ilivyooonyeshwa katika mchoro wa mduara . Magonjwa ya mwili , ingawa ni ya kweli , hasa ni dalili la tatizo la ndani - maisha ya ubinafsi . Viyvo hivyo matatizo ya kisaikolojia yalioonyeshwa katika maeneo ya "nafsi".



UZIMA WA MILELE (MAISHA KATIKA KRISTO)

Charles R. Solomon, Ed.D., is Founder and President of **Grace Fe**
P.O. Box 6115, Sevierville, TN USA 37862, Telephone 423-429-0450, F
Email—ChuckGFI @ AOL.COM

The pioneer of a Christ-centered approach to counseling called *Spi* written 7 books: *Handbook to Happiness, The Ins and Out of Rejection, Counseling, Handbook to Acceptance, Gems and Jargon* (out of print), and *Handbook to Happiness and You, A Spiritual Clinic.*

This tract is a condensation of Chapter 2 of *Handbook to Happiness* since the first printing in 1972. It may be obtained @ $0.25 per copy, alc or retail from: **Solomon Publications**, P.O. Box 6115, Sevierville,

Translated by Rev. Godson Mshana, P.O. Box 7183,

Ukombozi Wako

Dalili za kisaikolojia huanza kutoweka wakati mtu anapoona jinsi Mungu anaweza kushugulika na kiini cha tatizo kwa kuondoa ufalme wa maisha ya ubinafsi .

Mchoro wa Mstari waonyesha kanuni ya "maisha yatokayo katika mauti" &endash; Hii ni njia ya Mungu yakukomesha mgongano wa kindani .

Mstari uliolala unawakilisha uzima wa milele , maisha ya Kristo . Kwa kufafanua , milele yaoonyesha kutokuwa na mwanzo wala mwisho . Unapita mipaka ya wakati . Kwa vile Kristo ni Mungu , daima Ameishi na ataendelea . Maisha yake ni yeye yule , jana , leo na hata milele (Waebrania 13:8) . Kama inavyoonyeshwa katika mstari upande wa kushoto , Kristo " alifanyika mwili " (Yohana 1 : 14) na akaishi katika mwili wa mwanadamu kwa miaka 33 . Alisulubishwa , akazikwa na akafufuka kotoka wafu siku ya tatu (1 Wakorintho 15: 3-4) . Anaendelea kuishi hata leo (Waebrania 7:25) . Fahamu Yakuwa uzima wa milele sio tu ukweli wa sasa na wakati ujao kwa mwamini bali pia unajumuisha umilele uliopita .

Hadi tunapozaliwa mara ya pili (Yohana 3:3) hatumo katika maisha ya Kristo - uzima milele - bali tumo kiroho katika maisha ya mauti ya Adamu . Mmoja anaweza kuona wazi yakuwa ikiwa mmojapo wa mababu zetu , wakiwakilishwa na alama zilizoachana pembe mstari , angelikosekana sisi pia tungekosekana . Kuzungumza mwilini , maisha yetu yalianzia katika Adamu , kwa hivyo chochote kilichofanyika kwake kilifanyika kwetu pia . Alipotenda dhambi , tulitenda dhambi . Alipokufa (kiroho) , tulikufa ambavyo tungelikufa katika babu yetu angelikufa kabla kuzaa watoto . Kwa vile kifo cha kiroho ni kutengwa kwa Mungu , sisi zote tulizaliwa tumekufa (kiroho) . Tunahitaji msamaha wa dhambi zetu , lakini pia tunahitaji uzima . Bwana Yesu Kristo alikuja kutoa yote - kwa kufa kwa ajili ya dhambi zetu na kwa kutoa uzima wake wa ufufuo (Yohana 10:10) .

Iwapo wewe ni mkristo , tayari unafahamu haya . Yale ambayo hujafahamu ni yafuatayo :

Kwa mwamini kifo cha mwili ni mlango kutoka maisha duniani na uwepo wa dhambi na kuingia uzimani mbinguni katika uwepo wa

Mungu . Vivyo hivyo , aina ingine ya kifo ni mlango kutoka katika maisha ya dhambi ya Adamu na kuingia katika uzima milele wa Kristo .Mtu " anapozaliwa mara ya pili ", hufa papo hapo . Huzaliwa katika maisha ya Kristo , na papo hapo hufa kutoka kwa maisha ya Adamu .

Kristo huingia katika maisha yetu tunapomwamini na kuzaliwa mara ya pili , lakini hiyo sio yote . Tunafanywa pia " washiriki " wa maisha Yake &endash; uzima wa milele . Warumi 6 :3 yasema hatukubatizwa tu katika Yesu Kristo (maisha Yake) bali pia katika mauti yake . Hatuwezi kuishi maisha mbili yanayo hitilafiana kwa wakati moja &endash; maisha ya Adamu na maisha ya Kristo .

Utambulisho Wako

Tunapompokea Kristo kwa imani , ina maana mauti yake msalabani , inahesabika kama malipo ya dhambi zetu . Lakini ina maana zaidi . Ina maana pia tunaingia katika maisha mapya &endash; yanayo tanda milele katika wakati uliopita na katika wakati ujao . Kusema katika njia nyingine , tunabadilisha historia yetu katika Adamu &endash; iliyo nzuri na mbaya &endash; na kuchukua historia ya milele katika Kristo . Tunarithi familia ya " kizazi kipya "! kwa kufanyika washiriki wa maisha ya Kristo , twakuwa washiriki wa mauti yake , mazishi , ufufuo , kupaa na kuketi katika ulimwengu wa roho (Warumi 6 : 3- 6; Wagalatia 2: 20 ; Waefeso 2: 6).

Yeye ana uzima moja tu , na uzima huu ndio tunapokea tunapozaliwa mara ya pili (1 Yohana 5 : 11 -12) .

Ijapokuwa na hadi tufahamu kwa imani yetu yakuwa tulisulubishwa pamoja na Kristo , tutaendelea kujaribu kumuishia Kristo , kwa njia ambazo tulijifunza katika maisha yetu ya zamani ya ubinafsi . Migongano inayotokana na historia yetu katika Adamu itaendelea kutusumbua na kutushinda . Walakini , kwa imani , tunapotwaa mahali petu msalabani katika umoja wa mauti ya Kristo na ufufuo , ndipo &endash; hapo tu &endash; twaweza kwa kweli " kuenenda katika upya wa uzima " (Warumi 6 : 4b) ambapo " mambo ya kale yamepita ; tazama , yote yamekuwa mapya " (2 Wakorintho 5 : 17) .

Maisha ya msalaba (kufahamu na kujua kusulubishwa na kufufuka pamoja na Kristo) ni mlango wa kuingia katika maisha ya kuongozwa na Roho (Wagalatia 5 : 16) . Ni maisha yatokayo katika mauti , ushindi utokayo katika kushindwa &endash;

makusudi na jawabu kwa mateso katika maisha ya mwamini . Njia yetu ya kwenda msalabani , pamoja na msalaba wenyewe , ni njia ya mateso , lakini ndiyo njia ya pekee inayoelekeza kufikia mwisho wa mateso .

Je ! umechoshwa vya kutosha na mgongano wa kindani na kushindwa kila mara na unataka kukomesha yote kwa imani ? Je ! utayari kufa kwa yote uliyo ili uishi katika yote Yake ? Kufanya hivyo ni kubadilisha maisha ya ubinafsi kwa maisha ya Kristo na kujazwa au kuongozwa na Roho Mtakatifu . Kukataa kufanya hivyo ni kuendelea kuenenda katika mwili na kuhuzunisha Roho na kuendelea kwa mgongano , mateso na kushindwa .

Sala ya Wokovu

Kama umechoshwa na uchungu unaosababishwa na kutenda mambo njia yako , Kristo atakuweka huru iwapo kwa uaminifu utajitoa na kumkubali apate njia yake .

Iwapo hujawai kumpokea Kristo kama mwokozi wa maisha yako , hitaji lako la kwanza ni kuruhusu Mungu akuumbe upya kwa kukupa kuzaliwa kwa kiroho . Waweza kuzaliwa mara ya pili iwapo kwa uaminifu utaomba hivi : " Baba wa mbinguni , nimeona mimi ni mwenye dhambi , bado nipo katika maisha ya Adamu , na kwamba nimetenda dhambi . Naamini ulimtuma mwanao wa pekee , Bwana Yesu Kristo , kufa badala yangu kwa ajili ya dhambi zangu . Naamini pia alifufuka na sasa aishi , na sasa hivi nampokea rohoni mwangu . Najitoa kwake hivi nilivyo , vyote ninavyo na nitakavyo kuwa . Nageuka kutoka dhambi na njia zangu za uchoyo ili niishi maisha yangu mapya katika Kristo . Asante kwa kuniokoa . Amina ."

Sala ya Utambulisho

Iwapo umeomba " sala ya wokovu " , umezaliwa mara ya pili , kwani Mungu asema huwapa wote wamwaminio uwezo wa kufanyika wana wake (Yohana 1 : 12) .

Sasa , iwapo umeomba sala ya wokovu sasa hivi au wakati uliyopita , kuomba " sala ya utambulisho " yaweza kukusaidia kufurahia maisha ya Kristo yenye ushindi na amani . Kabla sala hii kutenda kazi , ni lazima umechoshwa kabisa na maisha yako ya ubinafsi ; lazima uwe umeshawishiwa na Roho Mtakatifu ubatili wa kuishi maisha ya Kikristo katika nguvu zako , na lazima uwe tayari kusalimisha uongozi wa maisha yako . Ikiwa hii ndiyo hali

yako , omba hivi .

" Baba , asante kwa kunisamehe dhambi zangu na kunitoa katika maisha ya Adamu na kunipandikiza katika maisha ya Kristo . Kwa vile sasa nimo ndani ya Kristo , naamini nilisulubishwa pamoja naye , nakazikwa naye , nikafufuka naye , na kwamba nimekaa naye katika mkono wako wa kuume . Kuanzia sasa na kuendelea , nachagua kuruhusu mwanao , Yesu Kristo aishi maisha yake ndani yangu na kupitia kwangu . Najihesabu nimekufa kwa dhambi na hai kwako , na nina mtegemea Roho Mtakatifu anikumbushe pale ninaposahau kufa kwangu pamoja na Kristo na kujaribu kuishi maisha kwa niaba yake katika hekima na nguvu zangu za kibinadamu . Nachagua kutoa utu wangu wote kama chombo cha haki, bila kuruhusu sehemu yeyote yangu kutumika kwa dhambi . Asante kwa kufanya Kristo na uzima wake hakika kwangu . Jitukuze kupitia kwangu . Kwa jina la Yesu naomba . Amina . "

[Charles R. Solomon , Ed . D ; ni Mwazilishi na Rais wa Grace Fellowship International (G.F.I) , P.O.BOX 6115 , Sevierville ,TN , USA 37862, Phone 433-429-0450 , Fax 423-429-0144 , Email : chuckgfi@aol.com Mungu alimpa wito wakuwa Mtangulizi wa Ushauri ambao Kristo ndiye ujumbe wa uhuru unaoitwa Spirituotherapy tangu mwaka wa 1967. Ameandika vitabu 7 katika lugha ya kingereza ; Handbook to Happiness , The ins and out of Rejection , Handbook for Christ - centred &endash; Counseling , Handbook to acceptance , Gems and jargon , Handbook to Happiness in verse na Handbook to Happiness and you , A spiritual Clinic .

Kijitabu hiki ni muhtasari ya sura ya pili ya kitabu , Handbook to Happiness . Karibu vitabu 300,000 vimeuzwa. Daktari John Woodward ndiye Mkurugenzi wa ushauri na mafunzo .

Kijitabu hiki kimetafsiriwa na Mchungaji Charles Ambaka , Mkurugenzi (GFI) Africa Mashariki , S.L.P. 8287 &endash; 00100 , Nairobi , Kenya , Akisaidiwa na Joseph Hiza na Angelo Kidava (Wazee wa Kanisa Nchini Jamuhuri ya Tanzania)]

Kwa mawasiliano zaidi,

Anwani ni,

Grace Fellowship International,

S .L. P. 8287 - 00100 Nairobi ,

Kenya.

Email: charlwema@yahoo.com

www.gracefellowshipintl.com